

GRADE 3 END TERM 3 DECEMBER 2021

KISWAHILI ACTIVITIES

1. UFAHAMU (Alama 10)

1. Soma hadithi kisha ujibu maswali yafuatayo. (alama 5)

Bi. Musa ana duka. Yeye huanza shughuli zake mapema ili wateja wake wampate dukani. Katika duka lake ameweka bei kwenye bidhaa na pia bidhaa zote zimepangwa kwenye rafu. Yeye hupima bidhaa zake kwa kutumia ratili. Bidhaa ambazo Bi. Musa huuza ni kama maziwa, mikate, mchele, sukari na chumvi. Bi. Musa huwakaribisha wateja wa ke vizuri.

a) Bi. Musa ana nini? _____

b) Yeye huanza shughuli zake saa ngapi? _____

c) Bidhaa zimepangwa wapi? _____

d) Andika vitu viwili ambavyo Bi. Musa huuza. (alama 2)

2. Soma hadithi kisha ujibu maswali yafuatayo. (Alama 5)

Bwana na Bi. Juma ni wakulima. Shambani mwao kuna mifugo na mimea ya aina tofauti. Bwana Juma hulima shamba lake kwa kutumia trekta. Wakati wa kupalilia wao hufanya kazi na watoto wao. Bwana Juma hutegemea shamba lake kwa mahitaji yake yote.

a) Bwana Juma hufanya kazi gani? _____ (alama 1)

b) Kwenye shamba lao kuna nini? _____ (alama 2)

c) Yeye hutumia nini kulima? _____ (alama 1)

d) Ni nani huwasaidia kupalilia? _____ (alama 1)

2. SARUFI **(Alama 15)**

1. Tumia kimilikishi sahihi kujaza pengo. **(alama 5)**

langu, yake, wako, chake

- a) Mkoba _____ utaanguka.
- b) Baba _____ alimpeleka shulenii.
- c) Jino _____ linauma.
- d) Kalamu _____ imepotea.
- e) Kikapu _____ kimepotea.

2. Tumia alama ya kiulizi (?) au kikomo (.) kukamilisha sentensi hizi.

(alama 5)

- a) Unataka nani
- b) Nilimtembelea nyanya
- c) Leo ni Jumapili
- d) Unaenda wapi
- e) Unaitwa nani

3. Kanusha sentensi hizi. **(alama 5)**

- a) Jana nilienda sokoni.

- b) Kesho nitafua nguo zangu.

- c) Leo ninamsaidia mama.

- d) Nilimtembelea babu shambani.

- e) Nitacheza na rafiki yangu.

3. KUANDIKA

(alama 10)

Andika insha kuhusu

"DARASA LANGU"

1. KUSIKILIZA NA KUZUNGUMZA

(Alama 5)

Sikiliza hadithi nitakayokusomea kisha nitakuuliza maswali.

Bi. Asha aliishi katika kijiji cha Bondeni. Yeye na mume wake walikuwa na watoto wanne. Waliwafunza watoto wao kuwa na maadili memd. Waliwafunza kuwa na heshima kwa wakubwa na wadogo wao. Watoto wao walipendwa na watu wote na walimu wao kwa sababu ya heshima.

- i) Bi. Asha aliishi katika kijiji kipi? _____
- ii) Bi. Asha alikuwa na watoto wangapi? _____
- iii) Bi. Asha na mume wake waliwafunza watoto wao nini?

- iv) Ni nani aliwapenda watoto wa Bi. Asha? (alama 2)

2. KUSOMA KWA SAUTI.

(Alama 10)

Soma hadithi hii kwa sauti.

Familia ya Kiprono iliishi jijini Nakuru. Kiprono alikuwa mtoto mzuri sana ambaye alipenda kuwasaidia wazazi wake kazi.

Siku moja baada ya kumaliza kazi za nyumbani, aliondoka kwenda kucheza. Baada tu ya kufunga mlango, kulitokea mtu mmoja akamshika kwa nguvu. Mtu yule alimlazimisha amfungulie mlango. Kiprono alikataa na kupiga mayowe. Kwa bahati nzuri babake alikuwa ametoka kazini. Kwa mbali alisikia mayowe na kukimbia. Alimkamata mtu yule na kumpeleka kwenye kituo cha polisi.